Website:www.jriiejournal.com ISSN 2520-7504 (Online) Vol.6, Iss.3, 2022 (pp. 421 - 427)

# Mwanamke Katika Bembelezi za Watikuu

**_Dr. Lina Akaka[1*] na Dr. Sheila Wandera- Simwa[2]_**

_[1*]Chuo Kikuu cha CUEA; Barua pepe: akakalina2016@gmail.com; Simu: 0710597991. ORCID iD: 0000-0003-4376-5794_

_[2]Chuo Kikuu cha Laikipia; Barua pepe: swandera@laikipia.ac.ke; Simu.:0722366005. ORCID iD: 0000-0002-5880-3493_

**_Abstract:_** _A culture of a people is embedded in their folklore and expressed through it. It also gives us a glimpse into their worldview and the way they interact, their beliefs and values. Lullabies are cultural songs sang worldover to soothe and lull crying children to sleep (Gunes na Gunes, 2012). Watikuu lullabies reflect the interactions of women for they are exclusively composed and sang by women. They are songs for women by women. Some of the lullabies sung, have been passed over from generation to generation. With regard to this, the women replace the content of the lullabies, while the melody remains. The Watikuu women compose new words depending on the message they want to pass across as they sing. There is always a target audience for the messages in the lullabies. Its in this context that the researchers investigated the messages especially those whose target audience are women in an attempt to find out how women perceive themselves among the Watikuu. Given that the composers and singers of the lullabies are women, the gynocritic theory was used to guide the analysis of a woman's perception of a woman in Watikuu lullabies._

**Keywords:** _Lullaby, Woman, Watikuu, Culture, Folklore_

**_Ikisiri:_** _Bembelezi ni nyimbo za kitamaduni zinazoimbwa kote ulimwenguni ili kuwabembeleza watoto wanaolia na kuwafanya walale, (Gunes na Gunes, 2012). Bembelezi za Watikuu huimbwa na wanawake. Baadhi ya bembelezi wanazoimba ni za kupokezwa kwa hivyo hufaraguliwa wanapoziimba. Hii ina maana kuwa wanawake Watikuu hutunga maneno upya ili kukidhi haja zao za kimawasiliano kutegemea ujumbe wanaotaka kuwasilisha wakati wanapoimba. Ujumbe huo huwa na mlengwa, ni kwa muktadha huu ambapo watafiti wanapania kuchunguza ujumbe hususan unaowalenga wanawake ili kubaini vile mwanamke anavyomwona mwanamke mwenzake katika jamii ya Watikuu. Kwa kuwa wazalishaji na waimbaji wa bembelezi hizi ni wanawake, nadharia ya uhakiki-kike itatumiwa kuchunguza mtazamo wa mwanamke dhidi ya mwanamke mwenzake na kwa jumla jinsi mwanamke anavyosawiriwa katika bembelezi za Kitikuu._

**_Maneno Muhimu:_** _Bembelezi, Mwanamke, Watikuu, Utamaduni_

**How to cite this work (APA):**

Akaka, L. & Wandera, S. (2022). Mwanamke katika bembelezi za Watikuu. _Journal of Research Innovation and Implications in Education_, _6_(3), 421 – 427.

## 1.Utangulizi

Simulizi za kitamaduni ni vyanzo vyenye utajiri wa mila, desturi, imani na utamaduni unaodumisha uhai wa maadili na ruwaza za tabia katika jamii za kiafrika (Dinslage, 2001). Simulizi hizi zinaweza kuwa methali, ngano, nyimbo hali kadhalika mashairi. Waafrika wana namna ya kubuni simulizi zilizosheheni vipengele mbalimbali vya utamaduni wao. Simulizi hizi huakisi pia mazingira na mwonoulimwengu wao. Lugha ndiyo chombo kinachotumiwa kubeba simulizi hizi kama anavyosema Kramsch (2014) kwamba lugha ndicho kifaa kikuu ambacho wanajamii hutumia kuendesha maisha yao. Kramsch anaendelea kufafanua kwamba inapotumiwa katika miktadha ya mawasiliano, hufumbatwa na utamaduni kwa njia nyingi na zenye utata. Bembelezi ni mojawapo ya simulizi zinazopatikana katika jamii za

kiafrika kando na methali, mashairi, ngano na aina nyinginezo za nyimbo.

Simulizi za waafrika zilikuwa chanzo kikubwa cha wanahistoria katika uratibu wa historia ya waafrika. Utafiti wa nyimbo za kitamaduni za jamii mbalimbali umechangia katika kuuelewa tamaduni mbalimbali, mitazamo ya jamii tofauti tofauti ya maisha kwa jumla na mitagusano ya kijinsia inavyojitokeza katika simulizi hizo. Lugha inayotumiwa katika bembelezi za Kitikuu inachangia pakubwa katika uelewa wa utamaduni na uhusiano wa wanawake katika jamii hii. Momanyi (2021) anasema kuwa lugha ni asasi mnamosafiria utamaduni wa jamii na kwamba lugha kama asasi ya jamii haiwezi kutenganishwa na utamaduni wa jamii husika.

## 2. Bembelezi

Bembelezi za Kitikuu, kama zilivyo bembelezi za jamii nyingine ulimwenguni huimbwa na wanawake na huzitumia kueleza dhiki za ndoa, hivyo kuwasaidia kutakasa hisia zao. Mackinlay na Baker (2005) wanasema akina mama wengi hupitia kwenye msongo wa mawazo, hofu na masikitiko ambayo yanaweza kupunguzwa kwa uimbaji wa bembelezi. Bembelezi huwa kama kitulizo na faraja kwa akina mama walio na matatizo hivyo uimbaji wake huwafaidi sio tu watoto bali mama zao pia.

Lugha inayotumiwa katika bembelezi za Watikuu huwa tata na yenye urejelezi na mafumbo mengi yaliyofumbata ujumbe unaowalenga wanajamii mbalimbali hususan wanawake, kando na watoto. Bembelezi zao huakisi vile jamii ya wanawake hutagusana pamoja na tajriba zao za mambo mbalimbali katika jamii na utamaduni wao kama wanawake. Bembelezi hizi huonyesha pia vile wanawake wanavyosawiriana wenyewe kwa wenyewe.

Baadhi ya ujumbe katika bembelezi za Watikuu uliomo hulenga watoto moja kwa moja. Hata hivyo kuna nyingine ambazo wanawake Watikuu huzitumia pia kama jukwaa la mawasiliano huku watoto wakifaidi tu kwa melodia zake. Wanawake wa Kitikuu hutumia bembelezi hizi kusemezana. Usemezano unaoendelea katika bembelezi hizi huonyesha bayana vile wanawake Watikuu huhusiana wenyewe kwa wenyewe. Kwa kuwa waimbaji wa bembelezi hizi huwa wanawake, makala hii inachunguza taswira ya mwanamke wa Kitikuu kutokana na vile anavyosawiriwa na mwanamke mwenzake.

## 3. Misingi ya Nadharia

Ingawa utafiti huu ni wa fasihi simulizi, nadharia inayohakiki kazi za fasihi andishi ilitumiwa kuongoza tahakiki hii. Hili si jambo geni, mara nyingi nadharia za fasihi na isimu hutumiwa kuhakiki vipera mbalimbali vya fasihi simulizi. Kwa hivyo nadharia ya uhakiki-kike ilitumiwa kuongoza uchunguzi wa bembelezi za Kitikuu katika makala hii. Nadharia hii ni kimelea cha nadharia ya ufeministi. Iliibuka wakati wa tapo la pili la nadharia kuu ya ufeministi. Nadharia ya uhakiki-kike huchunguza maandishi ya wanawake (Plate, 2016). Hata hivyo katika makala hii nadharia ya uhakiki-kike ilitumiwa kuchunguza nyimbo za fasihi simulizi za aina ya bembelezi. Matumizi ya nadharia zinazotumiwa kuchunguza kazi za fasihi andishi katika uchunguzi wa kazi za fasihi simulizi ni wa kawaida. Istilahi ya uhakiki-kike iliasisiwa na Elaine Showalter katika makala yake *"Toward a Feminist Poetics"* ya 1979. Nadharia hii huchunguza kazi za fasihi zilizoandikwa na wanawake kinyume na wanawake kama wasomaji wa kazi za fasihi. Uhakiki-kike ni vuguvugu lililoanzishwa kwa madhumuni ya kulenga utamaduni wa mwanamke na vile anavyoueleza mwenyewe (Plate, 2016). Ansari (2015) anasema wanauhakiki- kike hulenga kuunda nadharia mpya za uchanganuzi wa fasihi za wanawake na kuanzisha vielelezo vyenye misingi yake katika uchunguzi wa tajriba za wanawake badala ya kutumia nadharia na mikabala ya kiume. Katika makala hii, waandishi wanapania kuchunguza vile wanawake wanavyosawiriana katika bembelezi za Watikuu na utamaduni wao vile unavyojitokeza katika bembelezi hizi. Usawiri wa mwanamke kwa mtazamo wa mwanamke.

## 4. Mbinu za Utafiti

Bembelezi za Watikuu ndizo zilikuwa kundi lengwa la utafiti huu. Watikuu ni wenyeji wa kisiwa cha Faza katika kaunti ya Lamu. Ni wamojawapo wa makundi ya Waswahili. Bembelezi ishirini zilikusanywa katika vikundi lengwa viwili vya mijadala na sita zikateuliwa kimaksudi ili kutafitiwa. Bembelezi sita zilizoteuliwa ili kutafitiwa ni zile ambazo ujumbe uliomo ulilenga mwanamke. Data ya bembelezi hizo ilitafsiriwa kwa usaidizi wa wasailiwa wa utafiti huu na kuchanganuliwa kwa kutumia mhimili wa "usawiri wa utamaduni na tajriba za mwanamke kwa mtazamo wa mwanamke" wa nadharia ya uhakiki-kike.

## 5. Mwanamke katika Bembelezi za Watikuu

Kama ilivyotajwa awali, bembelezi za Watikuu huimbwa na wanawake. Bembelezi hizi kando na kubembeleza watoto ili watulie au walale, huwa na ujumbe ambao hulenga watu tofauti katika jamii. Wanawake katika jamii hii huzitumia kama jukwaa la kuwasilisha mawazo yao. Chiraghdin (1973) katika Abdallah (2012) anashadidia wazo hilo anaposema kwamba "Na mtu akiwa na dhiki ya moyo, hapana njia bora kuliko kulitoa alilonalo moyoni. Na kwa Mswahili, njia nzuri zaidi ni ya kutongoa kwa mashairi na nyimbo, akiwa ajua." Kwa mwanamke akiwa amekosewa na mwenzake, hutunga bembelezi ili kuwasilisha tetesi zake. Mwanamke ambaye ujumbe umelenga pia hujibu kwa bembelezi nyingine. Desturi ya wanawake wa Waswahili kutumia nyimbo kama jukwaa la mawasiliano ni la kawaida kama anavyosema Mwai (1997).

## 6. Mwanamke kama Mnafiki

Bembelezi ifuatayo iliimbwa na mwanamke ambaye alikosewa na rafiki yake wa karibu sana kama anavyoeleza kwamba alimpa rafiki yake siri za ndani. Imebeba ujumbe kwa rafiki wa kike wa mwimbaji. Utamaduni wa mwanamke mtikuu unabainika katika bembelezi hii. Katika ubeti wa kwanza, mwimbaji anasema alimpa rafiki yake siri zake za ndani lakini akaanza kumla ndani kwa ndani. Wakiwa marafiki, alikuwa akimpamba kwa wanja (pambo la macho). Hili linaonyesha utamaduni wa wanawake Watikuu wa mapambo ya mwili. Mwimbaji anamwona rafiki yake kama mnafiki. Walikuwa marafiki wa dhati hata akampa siri zake za ndani lakini akamsaliti. Jambo hili linaonyesha kuwa wanawake katika jamii hii hawawezi kuaminika. Urafiki wa karibu sana kama unavyoelezwa na mwimbaji unaweza kuishia katika kilio na majuto kama inavyodhihirika katika ubeti ufuatao:

*Nchocho howa nchocho howa x2*
*Nilikufanya rafiki kakupa siri za ndani*
*Kisha kakufanya wanda kakutia matoni*
Karama uwe ni simba hunila ndani kwa ndani

Ubeti wa pili ufuatao unaendeleza ujumbe wa ubeti wa kwanza. Mwimbaji alikuwa akimlaumu rafiki yake kwa kumpa mtoto wake wa kike mwanamume ndipo akasema "Karama wewe ni simba hunila ndani kwa ndani." Mwimbaji analalamika kuhusu uharibifu wa ubikra wa binti yake. Anatoa kauli zake kimafumbo kwa kuuliza ni nani atakayesoma karatasi iliyoloa maji. Maana ya kauli hii ni ubikra , kwamba atakayemwoa binti yake ni nani baada ya kuharibiwa ubikra na mwanamume ambaye alipewa na rafiki yake (mwimbaji). Kauli hii inaonyesha vile mwanamke mtikuu anavyothamini ubikra. Mwanamke anayeharibu ubikra wake kabla ya ndoa huwa na tatizo la kupata mume. Wanawake huiona thamani yao kwa wanamume ikiwa katika uhifadhi wa ubikra wao na unapoharibiwa kabla ya ndoa, huenda pasiwe na mwanamume wa kumwoa msichana kama huyo kama inavyodhihirika katika swali la mwimbaji katika mshororo wa kwanza wa ubeti ufuatao:

*Karatasi ya maini mwenye kusoma ni nyani?*
*Alonitakia imi ni mwanangu Asumani*
*Kuchukua va ahera kuvaeta duniani*

Katika ubeti wa tatu ufuatao, mwimbaji anamhimiza binti yake mdogo kukua ili amfundishe unyumba, amfundishe vile atakavyoishi na mume wake. Anamwuliza iwapo kuna mtu ambaye ameshamjua kimwili. Iwapo yupo, angemfunga kwa kufuli ili pasije mwingine akazifungua. Wanawake Watikuu wana jukumu la kuwausia binti zao kuhusu mambo ya unyumba. Majukumu ya wanawake kwa watoto na waume wao hayapatikani katika jamii ya Watikuu peke yao, fasihi simulizi zingine za kiafrika zinadhihirisha hilo pia (Wandera, 1996). Kwa mfano Lubuuka na Gakuo (2021) wanasema kuwa methali za Wanyankole zinaonyesha kwamba utamaduni umemtengea mwanamke majukumu ya malezi, kuelekeza na kufundisha watoto, kusafisha nyumba na kushughulikia maslahi ya mume wake. Mawazo yanashadidiwa pia na Kobia (2016) anapoonyesha vile methali za Waswahili zenye sitiari za kuku zinavyomwakisi mwanamke kimafumbo. Katika methali hizo mwanamke anaakisiwa kama mlinzi, mlezi na mwalimu wa watoto wake. Hali hii inaonekana pia katika bembelezi za Kitikuu mwimbaji anapomhimiza binti yake akue ili amfundishe unyumba katika ubeti ufuatao:

*Kua mwanangu Rukiya nikusomeshe skuli*
*Nikufundishe ubembe uhadaliye vavuli*
*Ni nyani afungudhieyeo nami nichie kufuli*

Mwanamke katika jamii hii angali amefungika katika majukumu aliyotengewa na jamii na ambayo yanaonekana kumkandamiza na kumweka chini ya mamlaka ya mwanamume. Watoto wa kike huanza kufundishwa kuhusu unyumba katika bembelezi wanazoimbiwa wakiwa wadogo na mafunzo hayo kuendelezwa zaidi unyagoni wanapovunja ungo. Kwa mujibu wa Momanyi (2021) mtoto wa kike hupitishwa kwenye hali hizi anapokua kupitia kwa asasi mbalimbali za kijamii kama vile desturi za kiutamaduni na za kidini. Hali hizi huathiri nafsi yake na kumfanya ajione kama raia wa daraja la pili ulimwenguni.

## 7. Mwanamke kama Hasidi

Akaka (2021) anasema jambo la mavyaa na mkazamwanawe kukosana si jipya katika jamii za kiafrika. Anahoji hali hii hudhihirika katika fasihi zao simulizi na andishi. Datta na wengineo (2003) wakinukuliwa na Akaka (2021) wanasema mizozo kati ya mavyaa na mkazamwana ni jambo la kawaida pia katika nchi za kiasia. Kwa mujibu wa wasailiwa katika utafiti huu, mwimbaji wa bembelezi ifuatayo hakuwa na uhusiano mzuri na mavyaa wake. Hali ambayo hutokea katika familia mbalimbali za Watikuu kwa mujibu wa wasailiwa. Mavyaa na wakazawana huonana kama wakewenza wa mume mmoja. Chuki hii hubuiliwa na sababu za kiuchumi. Kwa mujibu wa wasailiwa, mtoto wa kiume ambaye alikuwa akiikimu familia yake kabla ya kuoa hupunguza mapato kwa familia yake na kuanza kumtunza mkewe anapooa. Hili linapofanyika, mavyaa huanza kumchukia mkazamwana na kumwona kama chanzo cha upungufu wa usaidizi ambao familia yake ilikuwa ikipata kutoka kwa mwanawe.

Katika ubeti ufuatao, bembelezi inaanza kwa kibwagizo cha kumbembeleza mtoto, hata hivyo ujumbe unaofuatia unaelekezwa kwa mavyaa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Katika bembelezi zao, kulenga watu kimafumbo ni jambo la kawaida. Hili linashadidiwa na Saville- Troike (2003) anaposema washiriki katika tukio la mawasiliano

huweza kufasiri kikamilifu ujumbe katika tukio la mawasiliano iwapo wana habari za awali kuhusu jambo linalozungumziwa. Waliojua mzozo uliokuwepo baina ya mwimbaji na mavyaa wake walielewa mlengwa wa ujumbe uliomo hata ingawa hakutajwa kwa jina lake halisi. Mkazamwana anampa mavyaa wake jina bandia Tima Tumu ili kuepuka kumtaja moja kwa moja. Anasema mavyaa wake alimtukana si yeye tu bali watu wa kwao pia, wazee kwa watoto.

*Howa nchoncho howa x2*
*Yana Tima Tumu alinichukana*
*Hakuchusaza vazee kwa vana*
*Asojua ruli simpe maana*

Ubeti huo unabainisha dhahiri vile wakazawana na mavyaa zao wanavyohusiana katika jamii ya Watikuu. Kama ilivyotajwa awali, fasihi simulizi ni chombo kinachobeba utamaduni, mila na desturi za jamii husika. Katika bembelezi hii inabainika kwamba mwanamke anakuwa adui ya mwanamke mwenzake kwa misingi ya kindoa. Mwimbaji anaonyesha hii kwa kutoa hisia zake kuhusu mavyaa wake katika bembelezi anayoimba. Kwa hivyo, mwimbaji wa bembelezi hii anamsawiri mavyaa wake kama mwenye choyo, matusi, chuki na wivu.

## 8. Mwanamke kama Hasimu

Katika bembelezi ifuatayo, mwimbaji anawasuta mawifi zake kwa mambo wanayoyasema juu yake. Bembelezi hii inaonyesha uhusiano uliopo baina ya mawifi katika jamii hii; inaonyesha uhasama uliopo kati ya watu na mke wa kaka yao. Nyimbo za kiutamaduni za jamii yoyote ile huweza kufichua mitagusano kati ya wanajamii mbalimbali. Wazo hili linashadidiwa na Onwuegbuna (2012) anaposema ingawa nyimbo zina majukumu anuwai katika jamii, mara nyingi katika nyimbo za kiutamaduni ni ujumbe uliomo na shughuli za utendaji zinazoambatana nazo ndizo hufichua vile watu wanavyoishi na mwono-ulimwengu wao kwa jumla. Wazo hili linadhihirika katika bembelezi ifuatayo:

*Nchocho howa, nchocho howa x2*
*Kuna chungu kiandisiwa huchokocha siku zote*
*Mwishiza mai jabia na kuni makoko yote*
*Mja hupanga kupata huva hataki akose*

Ubeti huo unaonyesha kutoelewana kwa mawifi. Inaonekana mawifi zake humsemasema kwa watu wa nje. Bembelezi yenyewe imegubikwa sitiari ambazo wasailiwa walieleza maana zake. Mshororo wa pili wa *kuna chungu kiandisiwa huchokocha siku zote* kwa Kiswahili sanifu una maana ya chungu kilioandaliwa ambacho hutokota kila wakati. Wifi ambaye ni mwimbaji anaeleza kwamba anafahamu maneno ambayo mawifi wake, dada za mumewe husema juu yake huko nje. Kisha anawahimiza kutumia maji yote yaliyo kwenye jabia na kuongeza makoko yote ya kuni motoni ili wauchochee kuwaka ili chungu kipate moto na kutokota zaidi. Kwa kusema hivyo, mwimbaji anajaribu kuwajuza mawifi zake kwamba ana habari kuhusu mambo yote wanayoyasema. Ubeti huu unaonyesha vile mwanamke anavyomsawiri mwanamke mwenzake, kwamba ni mdaku na mwenye kusemasema mambo yasiyomhusu. Taswira inayojitokeza kuhusu wanawake hawa ni kwamba mawifi katika jamii hii hawana uhusiano mzuri. Kuna mambo ya kindoa ambayo husababisha mizozo kati yao. Kulingana na wasailiwa katika utafiti kutoelewana kwao husababishwa na mambo kama yale yanayoleta tofauti kati ya mavyaa na mkaza mwana.

Mabinti ambao hawajaolewa huwa wamemtegemea kaka yao kuwakimu kimaisha na anapooa wanaanza kumwonea wifi yao wivu hususan kaka yao akikatiza usaidizi aliokuwa akiwapa. Onwuegbuna (2012) alitaja kwamba nyimbo hufichua vile watu wanavyoishi. Naye Kayode (2013) anahoji kuwa kwamba ushiriki tendi wa wanawake katika uimbaji ni dhihirisho la mambo yanayofanyika katika jamii kwenye mifumo ya imani zao, maadili na utambulisho. Nzewi (1999) pia anasema maneno yaliyo kwenye nyimbo zao huakisi tajriba na maisha yao ya kila siku. Kwa hakika, haya wanayoyasema Kayode (2013) na Nzewi (1999) yanadhihirika katika bembelezi za Watikuu. Katika ubeti ufuatao wa pili, mwimbaji anaendelea kuwasuta akiwaambia wanajifanya wanajua mambo yote ila ni siasa tu zao zisizoisha.

*Muifanyiza wajuzi hapo siasa hamuziisi*
*Chungu mukiandisecho hulalamika vapishi*
*Mutazidi kutotea ama mutaveka iti*

Mwimbaji anawaambia wifi zake kimafumbo kuwa watu hulalamika kwa sababu ya maneno ambayo wanasema juu yake. Kwa hivyo anawauliza kama watazidi kusemasema au watakoma kusemasema juu yake. Bembelezi hii inaakisi uhasimu uliopo kati ya wanawake. Hii ina maana kuwa wanawake wenye uhusiano wa kindoa katika jamii hii hawana uhusiano mzuri. Kimsingi mwanamke mtikuu amesawiriwa kama mtu anayejiingizaingiza kwenye maneno yasiyomhusu.

## 9. Mwanamke kama Mlezi

Historia, utamaduni na mazingira ya jamii hufumbatwa katika fasihi simulizi zao (Nzewi, 1999). Utamaduni wa Watikuu wa kuusia mabinti zao unajitokeza katika bembelezi ifuatayo. Mojawapo ya majukumu ya akina mama wa Wakitikuu ni malezi ya mabinti zao, kuwaadilisha na kuwafundisha unyumba. Mafunzo ya kimaadili hupitishwa kwao kupitia kwa simulizi kama vile methali na nyimbo, bembelezi zikiwemo. Hili linadhihirishwa na Kobia (2016) anaposema akina mama wa kiafrika ndio walezi wa watoto. Watoto walilelewa kwa kupigiwa methali zilizosheheni semi za kimaadili, nyimbo zilizojaa wosia na hata kughaniwa ngano zilizosheheni mafunzo ya maadili (Wandera-Simwa, 2015). Desturi ya Waswahili kuwausia mabinti zao

inaonekana pia katika tenzi mbalimbali za Waswahili kama vile Utenzi wa Mwanakupona, Utenzi wa Hati, na Utenzi wa Kidani cha Huba (Wandera, 1996). Bembelezi za watoto pia zilitumiwa kupitisha ujumbe wa wosia kama inavyodhihirika katika ubeti ufuatao mwimbaji anapomuusia binti yake:

*Howa nchoncho howa x2*
*Bamba ni kitu muhimu kwa kusi na kaskazi*
*Na nyumba pia hudumu hupungua nyingi kazi*
*Waume hujifahamu mambo yote ni wazazi*

*Howa nchocho howa x2*
*Bamba ndilo la kufaa kwa mvua na hata jua*
*Nyumba ni yako haswa kwa mtu atakutowa*

Ubeti unaanza kwa mshororo wa kibwagizo mama akimwambia mtoto anyamaze. Mama anazungumza na mtoto katika bembelezi hii kimafumbo. Bamba katika muktadha wa bembelezi hii ni mume. Mwanamke wa Kitikuu huanza kuusiwa kuhusu unyumba mapema katika maisha yake kupitia kwa simulizi zao hadi anapovunja ungo. Wosia huu huendelea katika uanawari wake hadi anapoolewa. Mara nyingi katika wosia unaotolewa, mtoto wa kike huaambiwa kumtii mume wake, kujipamba kwa ajili yake na kumtumikia kwa njia zote. Kwa maneno mengine nafasi yake katika ndoa ni ya malezi ya mume na watoto wake. Momanyi (2021) anashadidia hilo anaposema kuwa mfumo wa kuumeni umetumiwa kama utaratibu wa masharti unaohalalisha asasi za kijamii zenye kuhimili tofauti za kiuana katika ugawaji wa kazi au shughuli.

Wanawake pia wanaonekana kukubali hali hii kama kudura yao maishani na hata kusaidia kuiendeleza. Katika ubeti huo, mwimbaji anamwambia binti yake kwamba mume ni mtu muhimu katika hali zote, hivyo anaelekea kumwambia kuwa hawezi kuwa na maisha mazuri bila mwanamume. Kwa hivyo, mwanamke wa Kitikuu katika bembelezi hii anasawiriwa kuwa mdhaifu. Usawiri huu unafanywa na mwanamke mwenzake hivyo wanawake wanajiona kama viumbe duni mbele ya wanaume. Utamaduni kama huu pamoja na mifumo ya kibabedume imemdhalilisha mwanamke kiasi cha kudunisha nafsi yake.

Ujumbe wa ubeti wa kwanza unaendelezwa katika ubeti wa pili. Mwimbaji anafafanua vile bamba, ambalo ni sitiari ya mwanamume litakavyomfaa binti yake. Bamba hilo litamfaa binti yake kwa mvua na jua. Mwanamke anasawiriwa na mwanamke mwenzake kama mtu asiyeweza kujikimu kimaisha bila mwanamume.

## 10. Mwanamke kama Kahaba

Katika bembelezi ifuatayo, mwimbaji mwenyewe anajisawiri kama kahaba. Mwanamke huyu aliachana na mume wake na kuolewa na mwingine kwa mujibu wa wasailiwa katika utafiti huu. Ubeti unaanza kwa kibwagizo, mama akimtuliza mtoto. Katika mshororo wa pili mwanamke huyo anaanza kutoa ujumbe kwa mumewe waliokuwa wametalikiana. Mume huyo aliitwa Simai. Kwa hivyo, anamwambia kila akipita awe akimsalimia na iwapo hatajibu salamu zake ajue kuwa hakusikia akimsalimia. Mshororo wa nne unaakisi mwanamke ambaye anaonekana kukiuka utamaduni wa jamii kwamba mwanamke daima awe chini ya utawala wa mwanamume. Mwanamke huyo anamwamrisha Boke mume wake wa pili kuondoka, kwa kuwa mume wake wa kwanza amefika. Anasema *“Nyuka utoke Mahadhi boke mekuzungukia.”* Kauli hii inabainisha kwamba baadhi ya wanawake katika jamii ya Watikuu huenda kinyume na utamaduni na kuonyesha sifa ambazo kwa muktadha wa utamaduni wao zinakaidi mila zao.

*Howa nchoncho howa x2*
*Simai ishe wanangu ukipita nivilia*
*Na kama sikukutika ni yiva sikukusikia*
*Nyuka utoke Mahadhi Boke mekuzungukia*

*Mwanahalima bahari mekosa kutanganyika*
*Nyumba hujenga jela na milango yake sita*
*Simai huvauyele na atakao akapita*

Katika ubeti wa pili, mwimbaji ambaye kwa jina ni Mwanahalima haoni haya kusema yeye ni bahari iliyokosa kutanganyika. Sitiari bahari imetumiwa kwa maana ya ukahaba. Kuna methali ya Waswahili isemayo *“Mtu halindi bahari ipitayo kila chombo.”* Methali hii inapiga mwangwi kauli za Mwanahalima katika mshororo wa kwanza wa ubeti wa pili. Mwanahalima anaendelea kueleza kwamba nyumba yake ina milango sita. Kwa mujibu wa wasailiwa wa utafiti huu, milango sita ni kauli ya kimafumbo ambayo ina maana kuwa wanaume hutoka na kuingia nyumbani mwake kila wakati. Kimsingi mwanamke katika bembelezi hii amejisawiri kama mkaidi mila, kahaba na mwenye nguvu za kuwadhibiti wanaume.

## 11. Mwanamke kama Adui ya Mwanamke

Mitagusano kati ya wanawake wa Kitikuu inaonekana pia katika bembelezi ifuatayo. Mwanamke wa Kitikuu katika bembelezi hii amesawiriwa kama mtu anayepokonya wenziwe waume. Mwimbaji wa bembelezi hii ni mwanamke anayelalamika kuhusu mwanamke aliyempokonya mume. Mwimbaji huyu anafumbata ujumbe wake kwenye mafumbo. Kwa kutumia mimea katika mazingira yake, anailinganisha na mume wake. Jambo hili linaonekana kushadidia mawazo ya Dinslage (2001), Kayode (2013), Wandera-Simwa (2015) na Lubuuka na Gakuo (2021), kwamba fasihi simulizi huakisi mazingira, utamaduni na mwono-ulimwengu wa jamii mbalimbali ulimwenguni. Katika bembelezi hii mazingira na utamaduni wa Watikuu unajitokeza.

*Nchocho howa nchocho howa x2*

*Nami nali nao wangu mbatata eeh*
*Katoka hasidi akaulizata*
*Naliliya yangu bahati kupata*

*Si bure mambo, nali nao wangu mkorosho*
*Katoka hasidi kaupiga moto*
*Naliliya yangu bahati ni chocho*

*Si bure mambo, usiku wa jana*
*Nilihangaika kaandika chai ndani ya*
*Birika eeh, nilidhani mbwangu kumbe*
*Ni bwa shirika*

Katika beti mbili za kwanza, mwimbaji anasema kuwa alikuwa na mbatata (matango) wake akatokea hasidi akaukanyaga. Wakati ambao mwanamke huwa ametumia katika kuutunza huu mmea hadi ukue na utoe matango mwingi. Shughuli hizo huanza kwa kutayarisha shamba, kupanda, kupalilia na kutia dawa na pengine kunyunyizia maji hadi matango yatakapofikia hatua ya kuvunwa. Hatua hizi zinalinganishwa na vile mwanamke hutenga wakati kumtunza mume wake. Hali hii inaonyesha ukweli wa mawazo ya Momanyi (2021) kwamba mifumo ya kibabedume katika jamii imemdhalilisha mwanamke kiasi cha kujiona duni mbele ya mume wake. Mwanamke basi hutwika jukumu la kumtunza mume. Katika bembelezi hii mwanamke anasawiriwa kama mlezi wa mume wake. Ubeti wa pili unasisitiza malezi hayo ila sasa mume analinganishwa na mkorosho uliokuzwa vizuri kisha akatokea adui akaupiga moto. Kulingana na wasailiwa wa utafiti huu adui aliyeupiga moto mkorosho huo na hasidi aliyeukanyaga mbatata ni mwanamke.

Mwanamke anayelengwa hapa alimnyang'anya mwimbaji mume wake. Katika ubeti wa tatu, mwimbaji anasema alihangaika kumwandalia mume wake chai ndani ya birika usiku wa jana akidhani ni wake peke yake kumbe alikuwa wa shirika. Jambo hili linaonyesha bayana vile wanawake hukoseana adabu wenyewe kwa wenyewe. Miongoni mwa wanawake Watikuu kuna wale ambao huingilia ndoa za wenzao na kuziharibu. Mwanamke amesawiriwa na mwanamke mwenzake kama mtu anayeharibu ndoa za wenzake. Mwanamke pia amejisawiri kama mtu ambaye amejitolea kama mlezi wa mume wake kulingana na vile walivyofunzwa na mama zao pamoja na utamaduni uliowalea (Wandera, 1996) .

## 11. Hitimisho

Makala hii ilichunguza vile mwanamke anavyosawiriwa na mwanamke katika bembelezi za Watikuu. Kimsingi, bembelezi hizi ni nyimbo za watoto. Hata ingawa ni nyimbo za watoto, Akaka (2021) anaonyesha kuwa ujumbe uliomo haulengi tu watoto bali watu wengine pia. Mtoto hufaidi tu kwa melodia zinazoambatana na bembelezi zenyewe zinapoimbwa. Waswahili wana ngoma na nyimbo za wanawake na wanaume. Miongoni mwa nyimbo zinazoimbwa na wanawake ni bembelezi. Kuna usemezano mwingi unaodhihirika katika bembelezi hizi. Waandishi walitafiti bembelezi ambazo ujumbe uliomo uliwalenga wanawake. Matokeo ya uchunguzi huo yanaonyesha kuwa wanawake husawiriana kwa njia mbalimbali. Mara nyingi wanawake hutatizika wanaposawiriwa kama makahaba na wanaume. Usawiri huo huonekana kutawaliwa na taasubi za kiume. Usawiri wa aina hiyo unatokea katika bembelezi za Watikuu pia, wanawake wenyewe wanaposawiriana vivyo hivyo.

Wanawake wanasawiriana kama watu wasioaminikia, watu ambao huharibiana ndoa. Kwa upande ule mwingine wanawake wanasawiriwa kama watu wanaozingatia utamaduni uliowalea katika ndoa. Mwanamke aliyepokonywa mume anaeleza alivyomtunza mume wake kama vile mtu atunzavyo mimea yake lakini akaja mwanamke mwingine akampokonya. Haya yanaelezwa kistiari lakini kimsingi ni kwamba katika bembelezi hiyo, wanawake aina mbili wanajitokeza. Mmoja anayezingatia utamaduni wa jamii kuhusu unyumba na mwingine mwenye kuharibu ndoa. Wanawake wamesawiriana pia kama wadaku, watu wa kusemasema maneno ya wenzao ovyoovyo bila sababu. Unafiki ni sifa inayopatikana miongoni mwa wanawake pia, hivyo wamesawiriwa kama wanafiki. Mwisho wanawake wanasawiriwa pia kuwa maadui wa wanawake wenzao. Kimsingi, bembelezi za Watikuu huimbwa na wanawake na baadhi ya diskosi zilizomo hulenga wanawake na kuonyesha vile wanavyotagusana katika jamii hiyo.

## Marejeleo


Akaka, Lina. (2021). *Sitiari na Ujumbe katika Bembelezi za Watikuu*. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Laikipia.

Abdalla, A. (2012). *Sauti ya Dhiki*. Oxford University Press.

Ansari, Gazala (2015). "The Role of Feminine in the Development of Feminist Literary Theories and Criticism." *In Research Journal of English, Language and Literature (RJELAL),* Vol. 3, Issue 4. Pp 95- 98.

Dinslage, Sabine (2001). "Traditional Education and Oral Literature: A Comparative Study of the Transmission of Moral Codes of Sexual Behavior in Folk Tales." In Kaschula, R. (ed). *African Oral Literature: Functions in Contemporary Contexts.* New Africa Books.

Kayode, M.S. (2013). African Folksongs as Veritable Resource Material for Revitalizing Music Education in Nigerian Schools, Research on Humanities and Social Sciences. Vol. 3, No. 10. Pp 30-37.

Kobia, J. M. (2016). "A Conceptual Metaphorical Analysis of Swahili Proverbs with Reference to Chicken Metaphor." *International Journal of Education and Research,* 4(2), 217- 228.

Kramsch, C. (2014). Language and Culture. *AILA review*, *27*(1), 30-55.

Lubuuka, Y. na Gakuo, J. (2021) "Itikadi za Kiuana katika Methali za Kinyankole." Katika *Taaluma: Jarida la CHAKITA.* Juzuu 1, Na. 1, Uk 119-129.

Mackinlay, E., & Baker, F. (2005). Nurturing Herself, Nurturing Her Baby: Creating Positive Experiences for First-time Mothers through Lullaby Singing, *Women and Music,* 9, 69- 89.

Momanyi, Clara. (2021) "Lugha na Uana: Sakata ya Nafsi." Katika *Taaluma: Jarida la CHAKITA.* Juzuu 1, Na. 1, Uk 1-7.

Mwai, K. W. (1997). The Power of Song for Swahili Women. Katika Kabira, W. M., Masinjila, M. & Obote, M. (eds). *Contesting Social Death: Essays on Gender and Culture.* K.O.L.A. 84- 102.

Nzewi, M. (1999). "Strategies for Music Education in Africa: Toward a Meaningful Progression from Tradition to Modern." *International Journal of Music Education,* (33) 72-87.

Onwuegbuna, I.E. (2012). "Music as an Embodiment of Culture and Philosophy: A Survey of Nigerian Folk Songs." In C. Krydz Ikwuemesi (ed). Pp 291-309. Enugu: ABIC

Plate, L. (2016). Gynocriticism. *The Wiley Blackwell Encyclopedia of Gender and Sexuality Studies*, 1-2.

Saville-Troike, M. (1982). The Ethnography of Communication. *Language in Society, 3,* 16(1), Pp 290- 314. Oxford: Basil Blackwell, Md: University Park Press.

Wandera, S.P. (1996). "*Usawiri wa Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili: 1800-1900:Uhalisi au Ugandamizwaji."* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Egerton

Wandera-Simwa, S.P. (2015) *"Taswira za jinsia katika Hadithi za Wanyala (Mumbo)"* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Laikipia.